**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI, KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA UDHIBITI WA FEDHA HARAMU NA MAPATO YATOKANAYO NA UHALIFU NAMBA 10 YA 2009.

Mheshimiwa Spika,

Awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye kustahiki kushukuriwa na viumbe vyote kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kukutana katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao ambapo leo tupo hapa kuupitia na kuujadili Mswada huu uliopo mbele yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuuchangia kwa umakini kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika,

Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako ili niwasilishe maoni ya Kamati yangu ya uchumi ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu Mswada wa sheria ya marekebisho ya sheria ya udhibiti wa fedha haramu na mapato yatokanayo na uhalifu namba 10 ya 2009.

Mheshimiwa Spika,

Kwa namna ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja Makamo wake wa kwanza Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wake wa Pili Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa ujasiri wao katika jukumu zima la kuiuongoza vyema nchi yetu sambamba na uendelezaji na uimarishaji wa sekta za Uwekezaji,Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika,

Naomba sasa nichukue fursa hii kuupongeza uongozi wa Afisi ya Rais Fedha na Mipango hususan Mheshimiwa Waziri Jamal Kassim Ali kwa uongozi wake bora, aidha nawapongeza wasaidizi wake na watalaamu wengine wa Wizara kwa mashirikiano na ufafanuzi walioutoa kwa kamati katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

Mheshimiwa Spika,

Napenda kuwashukuru Wanasheria wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati.

Mheshimiwa Spika,

Nitakuwa sijatenda haki iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati ya Uchumi kwa kazi nzito waliyoifanya ya kuujadili na kuuchambua mswada ulioletwa mbele yao kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Kwa heshima na taadhima, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti

2. Mhe. Juma Makungu Juma - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
6. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf - Mjumbe
8. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

Mheshimiwa Spika,

Katika uchambuzi wa Mswada huu, Kamati yangu haikusita kufanya kazi bega kwa bega na makatibu wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kuuchambua ipasavyo mswada huu, naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo;

1. Ndugu Noman Thabit Noman -Katibu
2. Ndugu Asma Ali Kassim -Katibu.

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuwa Mswada unaofanyiwa marekebisho umehusisha mambo mapya haswa yanahusiana na ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi, Kamati yangu ilipatiwa mafunzo kutoka Afisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar na kwa kushirikiana na watendaji kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu(FIU). Mafunzo hayo yalijikita katika kutambua mfumo mzima unaotumiwa na wahalifu wa makosa mbalimbali na kujipatia fedha kutokana na uhalifu wanaoufanya.

Mheshimiwa Spika,

Uhalifu wa utakatishaji wa fedha haramu huwa unahusisha makosa tangulizi ambayo makosa hayo husababisha mhalifu kujipatia Fedha na kujaribu kuzisafisha Fedha hizokwa kuziingiza kwenye mfumo rasmi wa kifedha kama vile kuziweka kwenye Benki mbalimbali za Ndani na Nje ya Nchi. Aidha, wahalifu hao huziwekwa fedha hizo kwenye vitega uchumi mbalimbali kwa ajili ya Uwekezaji. Makosa tangulizi yanayokwenda sambamba na makosa ya utakatishaji fedha haramu ni makosa ya Madawa ya kulevya, Rushwa, Wizi, Ujambazi, Makosa ya ukwepaji kodi, Uuzaji na Usafirishaji wa Silaha kinyume na sheria na makosa mengine yanoyofana na hayo.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yetu inaipongeza Serikali kwa kuleta mswada huu kwa hati ya dharura katika wakati mwafaka ambapo nchi yetu imo kwenye mageuzi makubwa ya kiuchumi kutoka uchumi wa kutegemea Utalii na Kilimo cha Mikarafu pekee hadi kwenda kwenye uchumi wa viwanda na uwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi waanzilishi wa Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika wa kupambana na utakatishaji Fedha Haramu (ESAAMLG) na kwa mujibu wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akiwasalisha Hotuba ya marekebisho ya mswada wa fedha haramu mnamo Febuari 2022 ndani ya Bunge la Tanzania alisema tathmini iliyofanywa na Umoja huo (ESAAMLG) ilibaini kuwepo kwa mapungufu makubwa kwenye sheria za utakatishaji wa fedha

haramu kwa upande wa Tanzania. Kutokana na mabadiliko ya viwango vya udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi na matumizi ya teknolojia mpya katika uhalifu ambapo sheria za awali za Tanzania hazikuzingatia mamba hayo na ndipo yakahitajika maboresho ya haraka.

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri wa Muungano na inapaswa kufuata masharti yote ya kimataifa ambayo Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania imeingia mikataba kama vile Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Kupambana na Utakatishaji Fedha Haramu (ESAAMLG) na Financial Action Force Standards (FATF), hivyo basi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar nayoinapaswa kubadilisha sheria yake ya udhibiti wa fedha haramu na mapato yatokanayo na uhalifu ili kuendana na matakwa ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika wa kupambana na Utakatishaji Fedha Haramu (ESAAMLG ) kwa kuingiza vipengele vipya vinavyohusiana na udhibiti wa ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi ili Zanzibar nayo iendane na mifumo ya kifedha ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika,

Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi inaendelea kuipongeza tena Serikali ya mapinduzi Zanzibar kwa kuchukua hatua za haraka katika kurekebisha kasoro zinazojitokeza kwenye sheria ya awali, Sheria ya Udhibiti wa fedha haramu na mapato yanayotokana na uhalifu Nam. 10 ya

mwaka 2009 kwa kuingiza vipengele vipya vya udhibiti wa ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi.

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuwa Serikali ya Zanzibar inayoongozwa na Dr Hussein Ali Mwinyi imedhamiria kuinua uchumi wa Zanzibar, uwepo wa Sheria na Sera zinazopambana na utakatishaji wa fedha haramu, udhibiti wa ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi itapelekea kutambulika Zanzibar kama ni sehemu salama kwa kuwekeza miradi mbalimbali hali ambayo itakuza uchumi wa Nchi na kuongezeka kwa soko la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika,

Kimsingi, Kamati yetu inakubaliana na dhana nzima iliyobebwa na mswada huu pamoja na marekebisho madogo iliyoyapendekeza wakati ilipokaa na Wizara kwa ajili ya kuupitia mswada huu. Marekebisho hayo yamegawika katika sehemu mbali mbali zikiwemo makosa ya kiuandishi, makosa katika uteuzi wa maneno, makosa ya kukosekana kwa baadhi ya vitu muhimu na vya msingi kuwemo katika mswada huu pamoja na kufuta baadhi ya maneno na vifungu.

Mheshimiwa Spika,

Kwa kuanzia na marekebisho ya kiuandishi, Kamati inapendekeza kifungu cha 3 cha mswada huu, kifanyiwe marekebisho kwenye tafsiri ya Maneno kama ifuatavyo:

i. Kwenye tafsiri ya neno “mteja” kwa kuongeza herufi “ku” baina ya neno “huduma” na “toka” ili kukamilisha neno “kutoka”.

ii. Kwenye tafsiri ya neno “mali za kimtandao” kwa kuongeza neno “au”baina ya neno “biashara” na “kuhamishwa”ili sentensi iweze kusomeka vizuri.

iii. Kwenye tafsiri ya neno “mtoa huduma za kimtandao” kwa kuongeza maneno “au kazi”baina ya neno “shughuli” na “zifuatazo” ili kuleta uwiano na tafsiri ya mswada wa lugha ya kingereza.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inapendekeza tafsiri ya neno “taasisi ya kifedha” ifutwe pamoja na vijalizo vyake vyote kwa vile tayari imo kwenye sheria inayorekebishwa ili kuepusha kujirejea kwa tafsiri hiyo. Aidha, maneno “taasisi ya kifedha” yaingie baina ya neno “taasisi ya usimamizi” na “mtoa taarifa” ili kuingia kwenye utaratibu wa ufutaji pamoja na maneno mengine.

Pia Kamati inapendekeza kufuta maneno “maana ya”yaliopo baina ya maneno “yake” na “mapya”kwenye ukurasa wa 96.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu inapendekeza kuongezwa kwa maneno “ufadhili wa ugaidi au ufadhili wa silaha za maangamizi” mwisho wa tafsiri ya “afisa mtoa taarifa za utakatishaji wa fedha haramu” ili kuleta uwiano baina ya nakala ya mswada wa Kiingereza na Kiswahili.

Mheshimiwa Spika,

Marekebisho mengine yaliyofanywa na Kamati yangu yameainishwa kwenye waraka wa marekebisho ambao tayari umeingizwa kwenye Baraza

Mtandao.

HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa nawashukuru Wajumbe wote kwa utulivu wenu na naomba tuuchangie, tuujadili, tutowe mapendekezo na hatimaye tuupitishe mswada huu kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati yangu, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………

Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani,
Mwenyekiti,
Kamati ya Uchumi,
Baraza la Wawakilishi,
Zanzibar.